# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## Uchambuzi wa Hotuba za Bajeti zilizowasilishwa Bungeni kwa Mtazamo wa Haki za Binadamu na Mlipuko wa Janga la Corona

Kituo cha Sheria na Haki za Bianadamu kinatoa taarifa hii baada ya kupitia hotuba za bajeti zilizozowasilisha katika Bunge la 11 mpaka Mei 6, 2020. Tunaamini kwamba, taarifa hii iliyochambua hotuba za bajeti zilizo wasilishwa itasaidia kufanya maboresho ya bajeti ya kila wizara pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Taifa itakayo wasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Philip Mpango ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. LHRC tunawapongeza mawaziri na watendaji wote wa wizara kwa maandalizi ya bajeti zilizowasilishwa Bungeni.

Uchambuzi huu unaweka mapendekezo ya kimkakati kufuatia uwepo wa maambukizi ya homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19). Hili limezingatia ukweli kuwa hakuna anayejua janga hili litaisha lini na utaacha madhara makubwa kwa kiasi gani. Hivyo, nchi inawajibu wa kuendelea na juhudi za kupambana na ugonjwa huu pamoja na kuweka mikakati itakayowezesha taifa kuendelea kipindi ambacho shughuli mbalimbali zimepungua kutokana na tishio la ugonjwa huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimepitia bajeti hii kwa kufuata Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 kama ilivyotumiwa katika hotuba mbalimbali za bajeti zilizowasilishwa Bungeni katika kipindi hiki.

Uchambuzi huu utakuwa wenye manufaa kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na naibu wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu


**Board of Directors:**

**Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member**

ya Bunge ya Bajeti, Mawaziri husika katika sekta zilizotajwa na Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu**

Maombi ya fedha katika hotuba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa yaboreshwe ili kuhakikisha kundi la watu wenye ulemavu wanapata huduma, taarifa na tahadhari mahususi za kujilinda dhidi ya ugonjwa wa Covid-19. Hii itaendana na kifungu cha 37 na 38 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, 2010 pamoja na Ibara ya 2,9 na 25 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2006. Ni wazi kwamba, kundi hili linahitaji mkakati maalumu katika mapambano dhidi ya virusi vya corona nchini. Hivyo, tunapendekeza bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu itenge fungu maalumu kwa ajili ya elimu, taarifa na huduma za kiafya kuendana na hali ya ulemavu husika tofauti na makundi mengine katika jamii.

**Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimepitia vizuri hotuba ya Waziri Viwanda na Biashara na kubaini mambo muhimu katika ukuaji wa sekta ya viwanda na biashara ambayo ikitekelezwa vizuri itainua pato la taifa kama ilivyoainishwa katika kitabu cha hotuba ya wizara hiyo. Pamoja na mambo hayo, ni vizuri kubainishwa kwamba hotuba ya bajeti hiyo inahitaji maboresho kuendana na janga lililopo kwa sasa katika taifa letu na dunia kwa ujumla.

Ikumbukwe kwamba, biashara na viwanda vimekumbwa na changamoto ya kushukuka kwa uzalishaji, mapato na ukuaji katika kipindi cha mwezi Februari mpaka mwezi Machi, 2020 mathalani biashara za mbogamboga na matunda zilishuka kwa kiwango cha asilimia 50 huku ununuzi wa zao la kakao lilishuka kwa kiwango cha asilimia 67.1.

Hii inaashiria namna ambayo mlipuko wa Covid-19 umeathiri sekta ya viwanda na biashara. Hivyo, taifa linahitaji kuweka mipango ya kimkakati kupambana na tatizo hili katika kila sekta.
Pamoja na juhudi zilizoelezwa na waziri husika, ni hakika kwamba bado kuna hitaji kubwa la vifaa kinga kwa ajili ya kupambana na janga hili. Kuna haja ya kuongeza viwanda vya kuzalisha vitakasa mikono, ikiwemo kutoa ruzuku katika viwanda hivyo ili kuweza kuongeza uzalishaji.

Mathalani katika ukurasa wa 58 wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni kielezo tosha kwamba kuna hitaji kubwa la vifaa hivyo.

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

*"Mpaka sasa, TIRDO imeweza kutengeneza* ***lita 202*** *za vitakasa mikono na kuwafikia watu mbalimbali kwa ajili ya matumizi"*. —Waziri wa Viwanda na Biashara.
Lita 202 ni chache ukilinganisha na mahitaji ya wananchi.

Pia, kuna hitaji la kuongeza uzalishaji wa barakoa na kusambaza kwa wananchi, viwanda vilivyopo sasa kama ilivyoanishwa katika hotuba ya bajeti vinahitaji kupewa ruzuku na serikali pamoja kusamehe tozo na kodi zinazohusiana na uzalishaji wa vifaa hivyo katika kipindi hiki. Matumizi ya vitambaa vya kawaida vinavyotumika na wananchi wengi kama njia ya kujikinga na virusi vya corona si salama ukilinganisha na barakoa maalum kwa ajili hiyo. LHRC tunatoa wito kwa Waziri wa Viwanda Mipango na Fedha kuona haja ya kuweka nguvu ili kuinua na kuchochea kasi ya uzalishaji wa vifaa hivi ili wananchi waweze kujilinda na kupunguza hatari ya maambuzi ya ugonjwa wa corona.

**Hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

**Gharama za huduma za mawasiliano katika kipindi hiki cha janga la corona**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano kuchukua hatua za makusudi ili kuchangia mapambano dhidi ya janga la virusi vya corona. Ni vema kwa Serikali kupunguza tozo katika makampuni ya simu ili kupunguza gharama za matumizi ya muda wa maongezi na huduma za mtandao '*internet'* kwa wananchi wenye ulazima wa kufanya hivyo ili kuendelea na shughuli za uzalishaji ambazo zina mchango wa moja kwa moja katika pato la mtu mmoja mmoja na pato la taifa.

Punguzo la tozo kwa makampuni ya simu katika kipindi hiki cha janga la corona litasaidia wananchi kufanya kazi na mawasiliano kwa njia ya mtandao ili kupunguza muingiliano wao katika sehemu mbalimbali na kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona. Katika wasilisho la hotuba ya bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano jambo hili halijawekewa msisitizo, hivyo tunapendekeza kwa Waziri wa Mipango na Fedha kuangalia jambo hili upya ili kupunguza muingiliano wa wananchi katika maeneo mbalimbali ikiwemo masokoni. Wananchi hasa wanaoishi maeneo ya mijini wataweza kufanya manunuzi kwa njia rahisi za kimitandao na njia ya kupiga simu, kuendelea na kazi wakiwa nyumbani bila kuhusisha muingiliano wa moja kwa moja kati ya mtu na mtu.

**Board of Directors:**
**Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member**

Hatua hii itasaidia nchi kupambana na athari za kiuchumi katika kipindi hiki cha janga la corona, kwani watu wataendelea kufanya kazi pamoja na kuwepo kwa janga hili. Kwa upande mwingine punguzo hili litasaidia idadi kubwa ya wanafunzi waliopo majumbani ili kuendelea kujifunza kupitia mitandao.

**Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**Kuongeza vituo vya kupima virusi vya corona nchini**

Januari 30, 2020, Shirika la Afya Dunian (WHO) lilitoa taarifa kwa dunia kwamba ugonjwa wa COVID-19 ni Dharura ya Jamii Kimataifa na hatimaye Machi 11, 2020, WHO ilitangaza ugonjwa huu kuwa ni janga la Dunia. Hivyo, nchi mbalimbali duniani zimeendelea kuchukua hatua za kupambana na ugonjwa huu ili kupunguza na kufuta kabisa kasi ya maambukizi ya ugonjwa huu.

Katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya, Serikali imeonesha hatua mbalimbali ambazo nchi inaendelea kuchukua ili kudhibiti kasi ya maambukizi, hadi sasa kuna maabara moja ya kupima virusi ya ugonjwa huu ambayo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyopo Dar es salaam pekee. Upatikanaji wa vitendea kazi kwa watoa huduma za afya ni muhimu sana kipindi hiki cha janga hili la corona. Tumeona changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa vifaa hivi kitu ambacho kinaweka watoa huduma wetu katika hatari ya maambukuzi. Hili linahitaji mkazo katika bajeti na kusimamia utekelezaji wake.

Elimu kwa umma kuhusu janga hili pia inahitaji msisitizo mkubwa. Wizara ishirikiane na wadau mbalimbali hasa mashirika yasiyokuwa ya serikali ili kuhakikisha elimu hii inafikia watu wengi ili waweze kujikinga.

Tunatoa wito kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongeza vituo vya kupima virusi vya ugonjwa huu ili wananchi kupima na kujua hali halisi ya idadi ya waathirika wa ugonjwa huu. Ni vema kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuona hitaji na kuweka pendekezo la kuanzisha maabara chini ya Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii kuongeza nguvu iliyopo sasa katika kituo kimoja kilichopo Dar es Salaam pekee. Hii itaongeza kasi ya

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member,
Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member,
Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

kutambua watu waliyoathirika na ugonjwa huu katika mikoa mbalimbali na kupata tiba kwa wakati.

i. **Mafunzo kwa watendaji wa mahakama za watoto**

Bunge limepitisha marekebisho ya Sheria ya Mtoto, Sura 13 yaliyofanyika mwaka huu ambayo yanaweka mamlaka katika Mahakama za Wilaya zote kuwa mahakama za watoto. Hivyo basi ni muhimu kwa Serikali kutenga bajeti maalaum kwa ajili ya kuongeza mafunzo ya masuala ya watoto kwa Maafisa wa Mahakama hizo ikiwemo maafisa ustawi wa jamii, mawakili, waendesha mashtaka, mahakimu na wanasheria kote nchini.

Kwa sasa bado kuna uhitaji wa mafunzo kwa maafisa hawa kama ilivyoanishwa katika hotuba ya Wizari ya Afya kuhusu namna bora ya kuendesha mashauri ya watoto katika mahakama za watoto kama ilivyoanishwa katika ukurasa wa 137 wa kitabu cha hotuba. Kwa kipindi hiki cha ugonjwa wa corona mafunzo haya yaanze kutolewa kwa njia ya mtandao ili kulinda maslahi mapana ya mtoto.

Kufanya hivi kutaifanya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendana na Miongozo ya Umoja wa Mataifa kuhusu utoaji haki katika Mahakama za watoto (Kanuni za Beijing).

ii. **Ukatili dhidi ya Watoto**

Kuongeza matangazo ya namna ambayo mtoto anaweza kufikia huduma ya simu kwa watoto *child help line* ili kufichua visa vya watoto walio katika hatari ya kupitia ukatili. Jitahada za sasa zilizofanywa na wizara ya afya ni za kupongezwa ingawa kunaitajika nguvu zaidi kwa ajili ya kuibua visa hivi vya ukatili dhidi ya watoto hususani katika kipindi ambacho mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yamepunguza kasi ya ufanyaji kazi kufuatia maambuziki ya ugongwa wa corona.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kitaendelea kutoa msaada wa kisheria kwa watoto na wananchi wote watakao ripoti kukumbwa na suala la ukatili katika maeneo mbalimbali nchini.

**Bajeti ya Wizara ya Elimu**

**Board of Directors:**
**Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatoa wito kwa Wizara ya Elimu na Serikali kupitia baadhi ya vipengele vya bajeti ya wizara ya elimu ili kuendeleza vizuri shughuli za kielimu katika kipindi ambacho nchi inapambana na virusi vya corona.

Serikali ichukue hatua za kukabiliana na janga hili, Wizara ya Elimu iongezewe bajeti ili kuanzisha *program* maalum kwa shule zote nchini kupitia njia ya teknolojia ili kufidia muda wa masomo katika wakati huu kwa njia ya radio na tv pamoja na njia nyingine za kimtandao kwa kuweka mpango maalumu. Ni wazi kwamba ratiba ambayo iko sasa katika radio na televisheni mbalimbali inaacha baadhi ya wananfunzi kwani hakuna ratiba moja ambayo wanafunzi wote wataweza kufuatilia kwa mujibu wa ratiba hiyo.

**Mwisho,** Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinashauri Serikali kufanya mambo yafuatayo;
(i). Kutoa tozo za kodi kwa wazalishaji wa dawa, vifaa tiba na vifaa kinga ili kuongeza unafuu kwa wananchi katika kupambana na magonjwa yanayoambatana na maradhi yanayosababishwa na virusi vya Corona.
(ii). Serikali kufanya tathimini ya mahitaji ya chakula pamoja na kuhakikisha uwepo wa akiba ya chakula katika kipindi ambacho dunia inapambana na maambukizi ya ugonjwa wa corona.
(iii). Serikali kuendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu wa bei za bidhaa kuwa imara kwa muda wote hususani kipindi hiki cha janga la corona.

**ZINGATIA: Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kitaendelea kufanya uchambuzi wa bajeti kadri zinavyowasilishwa na kutoa mapendekezo.**

**Board of Directors:**
**Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member**